# HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE UFUNGUZI WA JENGO JIPYA LA BENKI KUU TAWI LA MWANZA TAREHE 13 JUNI, 2021

*Mheshimiwa Dotto Biteko, Waziri wa Madini ambaye Anamwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango;*

*Dkt. Juma Malik Akili, Katibu Mkuu anayemwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar;*

*Waheshimiwa Mawaziri wengine mliopo;*

*Mheshimiwa Mhandisi Robert Gabriel, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na Wakuu Wa Mikoa Jirani mliopo;*

*Waheshimiwa Wabunge mliopo;*

*Ndugu Makatibu Wakuu mliopo;*

*Prof. Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania;*

*Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;*

*Viongozi wengine wa Serikali mliopo;*

*Viongozi wa Vyama vya Siasa mkiongozwa na Ndugu Christine Mndeme, Naibu Katibu Mkuu wa CCM na Ndugu Anthony Diallo, Mwenyekiti wa CCM – Mkoa wa Mwanza;*

*Ndugu Viongozi wa Dini mliopo;*

*Viongozi na Watumishi wengine wa Benki Kuu;*

*Viongozi wa Umoja wa Mabenki Tanzania;*

*Wageni Waalikwa, Wana-Habari, Mabibi na Mabwana;*

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kutupa uzima, afya njema na kutuweza tukutane hapa leo. Aidha, naushukuru Uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Benki Kuu ya Tanzania kwa kunikaribisha kwenye hafla hii ya uzinduzi wa Jengo hili jipya la Benki Kuu ambalo limegharimu **shilingi bilioni 42.1**, ambapo **shilingi bilioni 23.37** ni kwa ajili ya ujenzi na **shilingi bilioni 18.73** zimetumika kuweka mitambo na mifumo mbalimbali.

Nitumie fursa hii, hapa mwanzoni kabisa, kuipongeza sana Benki Kuu kwa kujenga Jengo hili zuri na la kisasa. Mbali na kuimarisha huduma za Benki Kuu kwenye Mikoa ya Kanda ya Ziwa (Mwanza, Shinyaga, Mara, Simiyu, Geita, Kagera na Kigoma), Jengo hili litaboresha mandhari ya Jiji la Mwanza. Na hii inaendana kabisa na dhamira ya Serikali ya

kulifanya Jiji la Mwanza kuwa kitovu cha Biashara kwenye eneo la nchi za Maziwa Makuu. Hata hivyo, nimenistushwa kidogo na gharama za ujenzi wa Jengo hilo; lakini leo sio wakati muafaka kulizungumza. Tutaliangalia huku mbeleni.

***Waheshimiwa Viongozi,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Majukumu ya Benki Kuu zote duniani, ikiwemo ya Tanzania, ni kuandaa na kutekeleza Sera ya Fedha (Monetary Policy) inayolenga uwepo wa utulivu wa bei kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa. Majukumu mengine mahsusi ni kama alivyoeleza Gavana:

(i) Kusimamia mabenki na taasisi za fedha na kuhakikisha uwepo wa utulivu katika sekta ya fedha;

(ii) Kusimamia utekelezaji, ufanisi na usalama wa mfumo wa malipo pamoja na masoko ya fedha nchini;

(iii) Kutunza akiba ya taifa ya fedha za kigeni;

(iv) Kuchapisha sarafu pamoja na noti na kuzisambaza;

(v) Kutunza amana za Serikali na za benki za biashara; na

(vi) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Serikali katika kuandaa na kutekeleza Sera za Uchumi.

Napenda nikiri kuwa, kwa ujumla, Benki Kuu ya Tanzania imejitahidi sana kutimiza majukumu hayo kikamilifu. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana na kazi nzuri iliyofanywa na Benki Kuu ni kuimarika kwa uchumi, ambapo kwa takriban miaka **5** iliyopita, uchumi wetu umekuwa kwa wastani wa zaidi ya **asilimia 6**. Na katika kuthibiti kuwa uchumi wetu umeimarika, mwaka jana (2020) mwezi Julai, Benki ya Dunia ilitutangaza kuingia Uchumi wa Kati wa Chini (*yaani Lower Middle Income*).

Uthibitisho mwingine umeonekana kwenye kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Corona, ambapo Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi chache duniani zilizoshuhudia ukuaji chanya wa uchumi wa **asilimia 4.8** mwaka 2020. Na hii ni dalili kwamba tumefanikiwa kujenga uchumi imara na ambao umechangamana (*diversified economy*).

Mafanikio mengine ni udhibiti wa mfumko wa bei ambapo kwa miaka mitano iliyopita ulikuwa wastani wa **asilimia 4.2**. Benki Kuu pia imeweza kudhibiti kushuka kwa thamani ya sarafu yetu, ambapo kwa miaka mitano iliyopita sarafu yetu ilibaki kuwa imara. Mwaka 2016/2017 thamani ya kubadilisha Dola moja ya Marekani ilikuwa **shilingi 2,230.1** lakini hadi kufikia mwaka 2019/2020 ilikuwa **shilingi 2,295.5**. Akiba ya fedha za kigeni nayo ipo imara, ambapo

mwezi Disemba 2020 ilikuwa **Dola za Marekani bilioni 4.767** ambayo inatukimu kununua bidhaa kwa **miezi 5.6**.

Sambamba na hilo, tumepiga hatua kubwa katika kuongeza idadi ya wananchi wanaotumia huduma rasmi za fedha (yaani *Financial Inclusion*) ambapo tumefikia **asilimia 65** na hivyo kutufanya tuwe miongoni mwa nchi zinazoongoza Barani Afrika. Na hapa nataka kumpongeza aliyekuwa Gavana wa Benki, Hayati Prof. Benno Ndulu kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye eneo hili; Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

Benki Kuu pia mmeweza kuimarisha usimamizi wa mabenki na taasisi za kifedha. Tumeshuhudia mara nyingi mkiingilia kati pindi mnapoona benki ama taasisi ya fedha inafanya kazi kwa kusuasua. Waswahili wanasema *"Chanda*

*chema huvikwa pete"*. Hivyo basi, napenda kutumia fursa hii kuipongeza Benki Kuu kwa kuwezesha kupatikana kwa mafanikio nilioeleza.

***Waheshimiwa Viongozi,***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, yapo baadhi ya maeneo machache ambayo natamani sana kuona Benki Kuu mnayapa mkazo zaidi.

***Mosi***, masharti magumu na riba kubwa zinazotolewa na Benki na taasisi za fedha nchini. Watanzania wengi wanashindwa kukopa kwenye benki na taasisi nyingine za fedha kutokana na masharti ya kukopa kuwa magumu na viwango vya riba kuwa juu. Mathalan, viwango vya kukopa kwenye benki ni kati ya **asilimia 12** hadi **asilimia 19**. Viwango hivi ni vikubwa sana kwa mtu wa kawaida. Lakini

tatizo la viwango vikubwa vya riba lilikuwa kubwa zaidi kwenye taasisi ndogo za fedha (yaani *microfinance institutions*), ambapo kuna wakati mtu alikuwa anaweza kukopa, kwa mfano, **shilingi milioni** moja; na akatakiwa kurejesha **shilingi milioni 1.5** katika kipindi cha miezi sita au chini ya hapo.

Hii ndiyo moja ya sababu, Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa, mwaka 2017, ilipitisha Sera, Sheria na Kanuni za Taasisi Ndogo za Fedha ili kuimarisha uratibu na usimamizi wa taasisi hizo. Lakini, pamoja na kupitishwa kwa Sera, Sheria na Kanuni hizo, zipo baadhi ya taasisi ndogo za fedha ambazo zinaendelea kutoza kiwango kikubwa cha riba. Hivyo, natoa wito kwa Benki Kuu kuendelea kuliangalia suala hili la riba ili kuwawezesha

wananchi, hususan ambao wako kwenye sekta isiyo rasmi kukopa na kuongeza mitaji yao.

Na katika hilo, nakumbuka, zamani tulikuwa tunaambiwa kuwa moja ya mambo yanayotajwa kuchangia riba kuwa juu ni kukosekana Mfumo wa Kumbukumbu za Mikopo na Madeni (yaani *Credit Reference Bureau*) kwa ajili ya kuwatambua wakopaji. Kwa sababu hiyo Benki na taasisi za fedha zilikuwa zinaweka riba kubwa ili kufidia pale inapotokea mikopo chechefu. Sasa Mfumo huo upo na unafanya kazi; lakini kama nilivyosema, viwango vya riba bado vipo juu. Hivyo basi, narudia kutoa rai kwa Benki Kuu kushughulikia suala hili. Kama Mfumo una matatizo, basi uimarishwe; lakini kama kuna matatizo mengine, na yenyewe yashughulikiwe ili viwango vya riba vishuke, angalau viwe chini ya **asilimia 10**.

***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Ukiachilia mbali kushughulikia tatizo la riba, nahimiza Benki Kuu kuweka mikakati ya kuhamasisha na kutengeneza mazingira mazuri kwa taasisi za fedha nchini, zikiwemo benki, kutoa mikopo ya muda mrefu. Benki nyingi nchini zinatoa mikopo ya muda mfupi. Kwa namna hii inakuwa vigumu sana kwa nchi yetu kukuza sekta za viwanda, kilimo lakini pia kuboresha makazi ya wananchi wetu. Kama mnavyofahamu, mikopo ya nama hiyo inahitaji muda mrefu.

***Tatu**,* nimewapongeza Benki Kuu kwa mafanikio mliyoyapata kwenye kuwezesha huduma jumuishi za kifedha kwa wananchi (*financial inclusion*). Hii imewezesha watu wengi, hususan vijana kuanzisha mifumo na biashara mbalimbali kwa njia ya kimtandao. Hata hivyo, ni vyema

sasa Benki Kuu ikaelekeza nguvu katika kuhamasisha matumizi kwa njia za kimtandao ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu. Hii sio tu itaongeza usalama wa fedha kwa wananchi wetu, bali pia itarahisisha biashara, ukusayaji wa mapato; na kupunguza gharama za uchapishaji fedha mara kwa mara. Na katika hilo, Benki Kuu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, hamna budi kukamilisha kwa haraka Mfumo wa Malipo ya papo hapo (*Tanzania Instant Payment System – TIPS*).

Sambamba na hilo, kuhusu *financial inclusion* pia, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, watu walioanzisha mifumo ama biashara za kimtadao wanapaswa kuwa na kanzidata mbili; moja ya kwao wenyewe na nyingine inatunzwa sehemu nyingine (*Redundancies*) ili itumike kama mbadala endapo kutatokea tatizo. Shida hapa ni gharama za utunzaji

kwenye Kanzidata mbadala kuwa juu. Hivyo basi, ningeshauri Benki Kuu mshirikiane na wadau wengine, ikiwemo Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuliangalia suala hili, na ili ikiwezekana, Kituo chetu cha Taarifa (*Data Centre*) kisaidie watu wa namna hiyo kupata huduma hiyo kwa gharama nafuu.

***Nne***, kama nilivyosema awali, mwezi Julai mwaka jana (2020) nchi yetu ilifanikiwa kuingia Kundi la Uchumi wa Kati. Kutokana na hatua hii, upo uwezekano kwamba, huenda misaada na mikopo yenye masharti nafuu ikapungua upande wetu. Hii inatuhitaji kuanza kuumiza kichwa katika kufikiria namna ya kupata fedha. Na katika hilo, naipongeza sana Wizara ya Fedha kwa kufikiria kuanzisha mchakato wa nchi yetu kufanyiwa Tathmini ya Nchi Kukopesheka (yaani *Sovereign Credit Rating*

*Assessment*). Hii itajenga imani kwa taasisi za fedha za kimataifa kuendelea kutukopesha. Lakini, zaidi yah apo, hatuna budi kuendelea na mbinu nyingine za kupata fedha, ikiwemo kutoa dhamana na hati fungani. Hata hivyo, kuhusu utaratibu huu wa dhamana na hati fungani, ni vyema tukawa makini ili tusiinyime fedha sekta binafsi. Kama mnavyofahamu, taasisi nyingi za fedha nchini, zimekuwa zikipendelea sana utaratibu wa kununua dhamana na hati fungani za Serikali kwa vile zinawapatia faida zaidi. Na hii ndiyo moja ya sababu inayofanya benki nyingi nchini kutotoa mikopo kwa wananchi na wafanyabiashara. Hivyo, ni vyema mambo haya yote yakayaangalia vizuri.

***Tano***; na mwisho lakini sio cha umuhimu, kama mnavyofahamu, tupo kwenye mapinduzi ya nne ya

viwanda yanayoongozwa na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Maendeleo haya yameleta mambo mengi duniani. Kwa mfano, kwa upande wa sekta ya fedha, tumeshuhudia kuibuka kwa sarafu mpya zinazotumika kwa njia ya kimtandao (*blockchain/crypto currency*). Najua bado nchi nyingi, ikiwemo Tanzania, hazijazikubali au kuanza kuzitumia sarafu hizo. Hata hivyo, wito wangu kwa Benki Kuu, ni vyema mkaanza kujitayarisha kwa maendeleo hayo. Kutokana na utandawazi, haitanishangaza kuona, Watanzania nao wakaanza kutumia fedha hizo za kimatandao. Hivyo, ili tusishtukizwe au kutanguliwa na wananchi wetu; ni vyema tukaanza kujiandaa mapema.

***Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango;***
***Gavana wa Benki Kuu;***
***Waheshimiwa Viongozi,***

***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Benki Kuu sio mahali pa maneno. Hapa ni mahala pa pesa na kuandaa Sera na mipango na mikakati ya maendeleo. Hivyo basi, nimaliziea kwa kuwashukuru Benki Kuu kwa zawadi ya sarafu mbalimbali mlizonipatia (*pesa mbili, pesa nne, nusu shilingi*, nk.). Aidha, nawapongeza wana-Kwaya wa Benki Kuu kwa burudani nzuri mliyotupatia.

Mwisho kabisa, narudia kuwashukuru kwa kunialika kwenye hafla. Nawapongeza kwa kujenga Jengo lenu Jipya; lakini pia kwa hatua mbalimbali zilizowezesha nchi yetu kupata mafanikio mengi makubwa ya kiuchumi. Wito wangu endeleeni kuchapa kazi kwa bidii huku mkitanguliza mbele maslahi ya taifa.

**Mungu Ibariki Benki Kuu!**

**Mungu Ibariki Tanzania!**

*Nawasalimu tena kwa Jina la Jamhuri*
*ya Muungano wa Tanzania!*

**"Asanteni Sana kwa kunisikiliza"**